**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAMBWE

**Mei,2026**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA**

**TANZANIA OFISI YA WAZIRI**

**MKUU –TAMISEMI**

**Nambaza Simu:-**

**Mkuu wa Shule 0759010817**

**Makamu Mkuu wa Shule 0758502692**

**Matron/Patron. 0766659653**

**Shule ya Sekondari Mambwe**

**S.L.P 95**

**Kalambo - Rukwa.**

**Tarehe 3.Mei. 2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………**
**…………………………………**
**S.L.P…………………………….**
**…………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAMBWE HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO MKOA RUKWA MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato chaTano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya PCM/HGL/HKL/HGLi/HGFa

Shule ya Sekondari Mambwe ipo umbali wa Kilometa 65 Kusini-Mashariki mwa Mji wa Matai na kilometa 98 kutoka kituo cha mabasi Katumba kilichopo Sumbawanga mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Katumba na stendi ya zamani Sumbawanga mjini kwa nauli ya Shilingi 8000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule ni tarehe ……………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……..............................

**Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

## 1.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili moja kijani na nyingine khaki kwa Wavulana. Iwe na rinda mbele na mkunjo chini (turn up) yenye mzunguko wa chini unaoanzia Sentimeta 16 hadi 19.

ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu;

iii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

iv. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;

v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vi. Sweta mbili kijani nyeusi zenye shingo‘’V’’ kwa ajili ya kujikinga na baridi

vii. Nguo za kushindia suruali mbili nyeusi na t-shirt moja yenye kola rangi ya kijani nyeusi Pia inaweza kupatikana shule kwa gharama ya Tsh.15,000 kwa watakaohitaji;

viii. Tai mbili yaani kijani nyeusi moja na khaki moja

ix. Tisheti (T-shirt) moja ya kijani iliyokolea yenye kola ( Pia inaweza kupatikana shuleni kwa gharama yaTSH 15,000 kwa watakaohitaji

**SARE YA MICHEZO.**

- Awe na physical training short(bukta) rangi bluu bahari (P.T.Short) na tracksuit rangi ya bluu bahari

.

- Raba jozi 01 kwa ajili ya michezo

## 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari (counter book) 8 aina quire 4;

ii. **Ream (A4) z**a Karatasi Mbili (2) kwa mwaka (moja kila muhula);

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;

iv. Scientific Calculator kwa masomo ya PCM na Geography (pia inaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya TSH 26,000 kwa atakayehitaji

v. Godoro moja la Ft 2.5 x6.

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, blanket1, foronya ya godoro1, chandarua 1 pembenne rangi ya bluu bahari.

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

x. Kwanja 1, rubber mopper 1, jembe 1 lenye mpini, reki 1 **(wanafunzi wa HGL)**

xi. Mifagio 2 wa ndani mmoja (soft bloom) na nje mmoja (chelewa wenye mpini), rubber mopper 1, kwanja 1 na jembe 1 lenye mpini (**wanafunzi wa HKL,HGFa, HGLi)**

**x.**Hard bloom1, jembe lenye mpini1, ndoo ya deki seti1 (mop na ndoo set) **(wanafunzi wa PCM)**

### 1.3 Michango mbalimbali

**a)Shule za Bweni**

| Na | Aina yaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- NB: Michango hii yote *Tsh.80,000/=* iingizwe kwenye akaunti NMB namba (62110003217 MAMBWE SECONDARY SCHOOL—EK) kisha uwasilishe risiti ya Benki shuleni wakati unaporipoti.

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kamailivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yoteinayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation studies);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Nimarufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini awapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Nimarufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Mwanafunzi anashauriwa kujiunga na bima ya afya ya jamii kwa kuchangia Tsh. 5,000 na kuunda kundi la wanafunzi 5 ili kurahisisha kupata huduma ya matibabu awapo shuleni.**

**2.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja,kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi isiyoruhusiwa;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA SEKONDARI MAMBWE**



**STANFORD H. KAMWELA**

**MKUU WA SHULE**




**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi**

**ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu nawatu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi/mlezi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBAZIFUATAZO:-**

- **Mkuu wa shule 0759010817**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0758502692**
- **Mwandamizi Taaluma 0766862587**
- **Mwandamizi Malezi 0738149826**

**OFISIYARAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI MAMBWE**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI**

**1. JINA KAMILI: ........................................................................................................................................(majina matatu au**

**kama yalivyotumika katika mtihani wa kidato cha nne, pia aje na results slip ya kidato cha nne)**

**2.JINA LA MZAZI/MLEZI: ........................................................................................................**

**3. MAHALI ANAPOISHI MZAZI/MLEZI ..........................................................................................**

**MAWASILIANO YA SIMU: .............................................................................................(Inayopatikana muda wote).**

**4. MAHALI ALIPOZALIWA MWANAFUNZI**

**i. Tarehe ya kuzaliwa: ..........................................**

**ii. Jinsi: ......................**

**iii. Kijiji/mtaa: ......................................................**

**iv. Wilaya: ............................................................**

**v. Mkoa: ......................................................................**

**5. DINI/DHEHEBU ....................................................................**

**(a) Shule ya Sekondari aliposoma ............................................................**

**(b) Mwaka wa kuhitimu kidato cha nne ....................................................**

**6. Je, ana ulemavu wowote au tatizo lolote la kiafya linalohitaji uangalizi maalumu ndiyo/hapana (kata isiyohusika)**

**Taja aina ya ulemavu kama ana ulemavu: ..........................................................................................**

**SAINI YA MWANAFUNZI: ................................................. TAREHE: ..................................................**

**SAINI YA MZAZI/MLEZI: ..................................................... TAREHE: .......................................................**

**NB: Fomu hii ijazwe Kwa uangalizi na kurudishwa shuleni.**

OFISIYARAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO

SHULE YA SEKONDARI MAMBWE

MKATABA.

Unashauriwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu.

SEHEMU A: MWANAFUNZI

Mimi......................................................... Nimesoma na kuelewa vizuri sheria, maagizo na kanuni zote za shule. Nakubali/sikubali nafasi hii na kuwa nitatumia uwezo wangu wote kujiendeleza kitaaluma, nitatii sheria, maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

SAHIHI………………………………..                                        TAREHE:…………………

SEHEMUB:MZAZI/MLEZI.

Mimi………………………………………………                    Mzazi/mlezi wa……………………………. Nimepokea taarifa ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari MAMBWE. Kwa kutambua umuhimu wa Elimu na wajibu wangu, naahidi kuwa muda wote mwanangu atakapokuwa shuleni nitashirikiana na Uongozi wa shule kumlea mtoto kwa kufuata sheria , maagizo na kanuni zote za shule na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya shule, nitatekeleza maelekezo yote yatakayotolewa na shule na nitatoa michango mingine yote ya shule iliyopitishwa kwa wakati.

SAHIHI………………………………..                                        TAREHE:…………………

MAMBWE SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 95,

MATAI,
KALAMBO–RUKWA.

DATE……………………………………………….
MEDICAL OFFICER:
………………………………………………………………
……………………………………………………………..
………………………………………………………………

REQUESTFORMEDICAL EXAMINATION

Please examine the above named as to His/Her fitness as indicated below. Arrange for necessary treatment sothatthe certificate may besigned and brought to school by the student. This certificate must be signed by aqualified medical officer of recognizedHospital ………………………………………………………………………………………………… ………

MEDICAL CERTIFICATE.

I have examined the above named student with regard to:-

Skin:…………………………………………..Abdomen……………………………….
Eyes: …………………………………………..Urine: ……………………………………..
Teeth:………………………………………….Hemoglobin:…………………………..
Spleen:………………………………………..Chest……………………………………..

Any Disabilities:……………………………………………………………………….

Iconsiderthat:-
He is in good health free from infections, and fit to come to school

He is fit to come to school after having:……………………………………………….
Treatment for:……………………………………………………………………………..

Name & Signature………………………………………. Date:………………………
MEDICAL OFFICER